





Chaku alipenda kucheza.


Alicheza uwanjani na wenzake.



Chaku alivutiwa na baiskeli ya Lila.
Lila ana baiskeli ya matairi matatu.




Chaku aliwaza kutengeneza baiskeli yake.




Chaku aliamua kuokota miti.



Alikumbuka kuwa
alihitaji nyundo na
misumari.




Chaku alikwenda kwa mjomba wake
kumwomba vifaa hivyo.




Mjomba wake alikubali kumpa vifaa.
Alimwambia Chaku awe mwangalifu
na vifaa hivyo.

Chaku aliwaza jinsi baiskeli
yake itakavyokuwa.






Chaku alianza kutengeneza balskeli yake. Aliitengeneza kwa uangalifu.



Baiskeli ya Chaku haikuwa imara sana.




Lila aliona jitihada za Chaku. Aliamua kumsaidia kuimarisha baiskeli.

Baiskeli ya Chaku imekuwa
imara sasa.





Chaku na Lila walifurahi.



Chaku aliendesha
baiskeli kila mahali
alipokwenda.

